# ULEZI

(Sehemu ya 7 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa | |
| 2. Jina la Mlezi wako<br>2.1 Jina | |
| 2.2 Anwani | |
| 2.3 Simu | |
| 3. Serikali yako ya huduma za jamii inayowajibika. | |

## Je! Ulezi ni nini?

Chini ya sehemu ya 7 ya Sheria ya Afya ya Akili 1983, watu walio na shida ya akili wanaweza kupewa mlezi wa kuwasaidia, ikiwa madaktari wawili wamesema inahitajika.

Mlezi wako anaweza kuwa serikali yako ya huduma za jamii, au mtu aliyeidhinishwa na serikali ya huduma za jamii. Ikiwa mlezi wako sio wa serikali ya huduma za jamii, naaitwa “mlezi wa kibinafsi”.

Mlezi wako ana nguvu za kisheria kukaumbia:

- mahali unapaswa kuishi
- mahali unapaswa kuhudhuria miadi ya matibabu ya dawa, kazi, elimu au ufunzi katika mahali palipowekwa na wakati uliowekwa.
- kuruhusu daktari au mtu mwingine aliyetajwa kukuona.

## Je! ninahitaji mlezi kwanini?

Madaktari wawili wanafikiria kuwa unahitaji usaidizi kuishi katika jamii kwani unayo shida ya akili na unahitaji mlezi kwa maslahi yako mwenyewe au kwa kulinda watu wengine.

## Je! wanakaa kwa muda gani?

Walezi hukaa hadi miezi sita wakati wa kwanza.

Ulezi wako anaweza kubadilishwa kwa muda mwingine wa miezi sita, na tena kwa muda mwingine wa mwaka moja kwa wakati moja, ikiwa daktari wako anayewajibika au mhudumu wako mteule anafikiria hii inahitajika. Watakuzungumzia kuhusu haya hivi karibuni.

Daktari wako anayewajibika ndiye daktari, au mtu mwingine, aliyeulizwa na serikali ya huduma za jamii kusema kama bado unahitaji mlezi. Ikiwa una mlezi wa kibinafsi, hii itafanywa na daktari anayeitwa badala yake "mhudumu mteule wa kimatibabu".

## Je! ninaweza kuomba rufaa?

Ikiwa unataka kuwacha kuwa na mlezi, unapaswa kuzungumza na mlezi wako, mfanyikazi wako wa jamii, daktari wako anayewajibika au mhudumu mteule wa kimatibabu.

Unaweza pia andikia serikali ya huduma za jamii kuwauliza wawachishe ulezi wako. Mtu kutoka serikali ya huduma za jamii anaweza kutaka kukuzungumzia kabla ya kuamua kama bado unahitaji mlezi.

Jamaa wako wa karibu zaidi anaweza kuachisha ulezi wako kwa kaundikia serikali ya huduma za jamii. Kijikaratasi hiki kinafafanua zaidi jamaa wako wa karibu zaidi ni nani.

Unaweza pia zungumza na Mahakama kusema kuwa haupaswi kuwa na mlezi tena.

## Mahakama ni nini na nini hufanyika?

Mahakama ni jopo la kujitegemea ambalo linaweza kuamua kama bado unahitaji mlezi. Itafanya mkutano na wewe na wafanyikazi wanaokujua kutoka kwa hospitali hiyo. Mkutano huu unaitwa " usikilizaji". Unaweza kumuuliza mtu mwingine aje kwenye usikilizaji huo kukusaidia. Kabla ya usikilizaji, washiriki wa Mahakama watasoma ripoti kukuhusu na utunzaji wako kutoka kwa hospitali. Mmoja wa washiriki wa mahakama pia watakuja kuzungumza nawe.

## Je! ni lini ninaweza kutuma ombi kwa mahakama?

Unaweza kutuma ombi kwenye Mahakama mara moja wakati wowote katika miezi sita ya kwanza ya ulezi wako. Kisha unaweza tuma ombi tena wakati wa miezi sita inayofauta kisha mara moja kila mwaka ambao uko bado chini ya ulezi.

Ikiwa unataka kuomba kwa Mahakama unaweza kuandika kwa:

The Tribunals Service
PO BOX 8793
5th Floor
Leicester
LE1 8BN Simu 0845 2232022

Unaweza kumuuliza wakili aandikie Mahakama kwa usaidizi wako katika usikilizaji. Serikali ya huduma za jamii na Shirika la Sheria wana orodha ya wakili ambao wana utaalam katika haya. Hautahitajika kulipa kwa usaidizi wa wakili kwa haya. Ni bure chini ya Mpango wa Usaidizi wa Kisheria.

## Kumjulisha jamaa wako wa karibu zaidi

Nakala ya kijikaratasi hiki itapewa mutu ambaye Sheria ya Afya ya Akili itasema kuwa ndiye jamaa wako wa karibu zaidi.

Kuna orodha ya watu katika Sheria ya Afya ya Akili ambao wanachukuliwa kama jama. Kwa kawaida, mtu anayekuja juu kabisa kwenye orodha ndiye jamaa wako wa karibu zaidi. Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kukupa kijikaratasi kinachoeleza haya na ni haki gani jamaa wako wa karibu zaidi anazo kuhusiana na utunzaji na matibabu yako.

Katika hali yako, tumeambiwa kuwa jamaa wako wa karibu zaidi ni:

| |
|---|
| |

Ikiwa hautaki huyu mtu apokee nakala ya kijikaratasi hiki, tafadhali mjulishe mlezi wako, mfanyikazi wa jamii au mtu aliyekupa kijikaratasi hiki.

Ikiwa haufikirii kuwa mtu huyu anafaa kuwa jamaa wako wa karibu zaidi, unawezaomba mtu mwingine achukuliwe kama jamaa wako wa karibu zaidi badala yeke kwenye Korti ya Mkoa. Serikali yako ya hudima za jamii inaweza kukupea kijikaratasi hiki kinachofafanua haya.

## Kanuni za Kufanya kazi

Hii ni Kanuni ya Kufanya kazi ambayo inakupa ushauri kuhusu Sheria ya Afya ya Akili kwa watu wanaohusika katika utunzaji wako. Wafanyikazi wanapaswa kuzingatia Kanuni inasema nini wakati wanapofanya uamuzi kuhusu utunzaji wako. Unaweza kuuliza nakala ya Kanuni, ikiwa unataka.

## Usaidizi na habari zaidi

Ikiwa kuna jambo lolote ambalo hauelewi kukusu utunzaji wako, tafadhali muulize mlezi wako, mfanyikazi wako wa jamii au mtu mwingine anayehusika katika utunzaji wako. Tafadhali uliza mfanyikazi kukufafanulia ikiwa kuna jambo lolote katika kijikaratasi hiki ambalo hauelewi au ikiwa una maswali mengine ambayo kijikaratasi hiki hakijajibu.

Tafadhali uliza nakala nyingine ya kijikaratasi hiki ukitaka kumpa mtu mwingine.